**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA ISHIRINI

## KIKAO CHA KUMI NA TISA

**02 JUNI, 2015**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA ISHIRINI

### KIKAO CHA KUMI NA TISA – TAREHE 02 JUNI, 2015

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### WAZIRI WA MAJI:

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha, 2015/2016.

### WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha, 2015/2016.

### MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha, 2014/2015 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2015/2016.

## MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha, 2015/2016.

## II. MASWALI:

### OFISI YA WAZIRI MKUU:

**126. MHESHIMIWA DKT. ANTONY GERVASE MBASSA (BIHARAMULO MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Kuna baadhi ya maeneo vijijini mara pampu za visima zinapoharibika au kupata hitilafu husababisha Wananchi kukosa huduma ya Maji Safi na salama:-

(a) Je, mamlaka husika huwa zina utaratibu upi wa kusimamia matengenezo ya pampu hizo;

(b) Pale inapotokea pampu imeibiwa na mwizi na mwizi akakamatwa na kushitakiwa na hatimaye kushinda kesi au kukosekana ushahidi; Je, mamlaka inachukua jukumu gani la kuwasaidia wananchi.

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

## WIZARA YA UJENZI:

**127. MHESHIMIWA DKT. CYRIL AUGUST CHAMI (MOSHI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali itaanza lini utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Old Moshi katika Jimbo la Moshi Vijijini.

**128. MHESHIMIWA SAID JUMA NKUMBA (SIKONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-
Barabara ya Tutuo – Ibumba kupitia Izimbili – Usoke na ile ya Sikonge – Mibono – Kipiri zilipandishwa hadhi kuwa barabara za Mkoa:-

(a) Je, matengenezo makubwa ya barabara hizo hasa eneo la Mibono – Kipiri ambalo halijatengenezwa kabisa yataanza lini;

(b) Je, Serikali inakubali kuwa barabara ya Sikonge – Mibono – Kipiri inahitaji fedha nyingi hivyo itengewe fedha za kutosha bajeti ya mwaka huu.

## WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

### 129. MHESHIMIWA MARTHA MOSES MLATA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:- Wizi wa kazi za wasanii bado ni tatizo sugu nchini:-

(a) Je, ni lini Serikali italeta Muswada Bungeni utakaobadilisha Sheria ya COSOTA ambayo imepitwa na wakati;

(b) Je, Serikali inafahamu kuwa kwa kutowashirikisha TRA katika usambazaji wa kazi za Wasanii inapoteza mapato mengi.

### 130. MHESHIMIWA HERBERT JAMES MNTANGI (MUHEZA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:- Waliokuwa wafanyakazi wa shamba la mpira Kihuhwi Wilayani Muheza walishinda kesi na wanatakiwa kulipwa mafao yao ambapo **PSRC** ilikabidhiwa jukumu la kusimamia shamba hilo na kuahidi kusaidia kulipa; na **CHC** ilipochukua jukumu toka **PSRC** iliahidi kusaidia kulipa lakini mpaka sasa hakuna malipo na shamba limekabidhiwa Taasisi chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba kutosimamia malipo ya mafao hayo kutolewa ni kudharau maamuzi ya mahakama;

(b) Kwa kuwa Serikali ndio iliyowatafuta wawekezaji wa shamba hilo na kuahidi kuwafuatilia hata nje ya nchi kushindwa; Je, kwanini Serikali isichukue jukumu la kuwalipa Wananchi hao.

**WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

**131. MHESHIMIWA ALIKO NIKUSUMA KIBONA (ILEJE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika:- Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa wamenunua Mahindi Wilayani Ileje kupitia Soko la Isongole bila kulipa ushuru wa zaidi ya Shilingi milioni mia mbili (200,000,000/):-

Je, ni lini Serikali italipa ushuru huo ambao ni muhimu kwa uendeshaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ileje ambayo haina wigo mpana na vyanzo vingine vya mapato.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**132. MHESHIMIWA CHRISTOWAJA GERSON MTINDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kituo cha Polisi cha Tarafa ya Ihanga Wilaya ya Ikungi ni cha muda mrefu na kinahudumia Wananchi wa Tarafa nzima:-

Je, ni lini Serikali itakipatia umeme kituo hicho.

**WIZARA YA ARHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**133. MHESHIMIWA RUKIA KASSIM AHMED (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

(a) Je, kwa nini Shirika la Nyumba la Taifa (N.H.C) hulazimisha watumishi wanaotaka kununua nyumba za Shirika wakope Benki badala ya kukatwa kwenye mishahara yao;

(b) Je, Serikali haioni kuwa kwa kufanya hivyo kunaongeza gharama zaidi ya 50% na kuzifanya nyumba hizo zisinunulike.

**WIZARA YA MAJI:**

**134. MHESHIMIWA VICENT JOSEPHAT NYERERE (MUSOMA MJINI)**:

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Mamlaka nyingi za maji mijini zinaendesha kwa shida sana kutokana na ukweli kwamba Serikali hailipi madeni ya huduma wanayopewa na mamlaka hizo:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kutoa ruzuku kwa mamlaka hizo ikiwemo MUWASA ili ziweze kujiendesha na kupunguza mzigo kwa Wananchi;

(b) Je, ni sawa Wizara na Idara za Serikali kama vile JWTZ, Polisi, Ikulu, (Nyumba za Wakuu wa Mikoa) kukatiwa maji kwa kushindwa kulipia huduma hiyo.

**III. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**DODOMA**
**02 JUNI, 2015**

**DKT. T. D. KASHILILAH**
**KATIBU WA BUNGE**